

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA WANAFUNZI
KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA PILI (FTNA) 2019**

021 KISWAHILI

BARAZA LA MITIHANI LA TANZANIA



**TAARIFA YA UCHAMBUZI WA MAJIBU YA
WANAFUNZI KATIKA UPIMAJI WA KIDATO CHA
PILI**

(FTNA) 2019

021 KISWAHILI

Kimechapishwa na:
Baraza la Mitihani la Tanzania,
S.L.P. 2624, Dar es Salaam
Tanzania.

© Baraza la Mitihani la Tanzania, 2020

Haki zote zimehifadhiwa.

YALIYOMO

DIBAJI.....	IV
1.0 UTANGULIZI.....	1
2.0 TATHIMINI YA KILA SWALI	2
2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO	2
2.1.1 Swalii la 1: Ufahamu	3
2.1.2 Swalii la 2: Ufupisho	9
2.2 SEHEMU B: SARUFI.....	13
2.2.1 Swalii la 3: Uundaji wa Maneno	13
2.2.2 Swalii la 4: Aina za Maneno	19
2.3 SEHEMU C: MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA.....	25
2.3.1 Swalii la 5: Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali.....	25
2.3.2 Swalii la 6: Lugha ya Kimazungumzo	29
2.4 SEHEMU D: FASIHI KWA UJUMLA	33
2.4.1 Swalii la 7: Fasihi Kwa Ujumla.....	33
2.4.2 Swalii la 8: Fasihi Simulizi.....	36
2.4.3 Swalii la 9: Fasihi Simulizi.....	40
2.5 SEHEMU E: UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI	44
2.5.1 Swalii la 10: Uandishi	44
3.0 UCHAMBUZI WA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MADA	49
4.0 HITIMISHO	50
5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO	51
KIAMBATISHO A	51
KIAMBATISHO B.....	53

DIBAJI

Baraza la Mitihani la Tanzania limeandaa taarifa ya uchambuzi wa majibu na viwango vya kufaulu vya wanafunzi katika Upimaji wa Kidato cha Pili mwaka 2019 kwa somo la Kiswahili. Taarifa hii ni tathmini endelevu inayooonesha mafanikio katika ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha Kwanza na cha Pili. Aidha, uchambuzi wa majibu ya wanafunzi katika upimaji huu ni uthibitisho wa maarifa waliyopata au waliyoshindwa kupata katika elimu ya Sekondari kwa Kidato cha Kwanza na cha Pili.

Uwasilishaji wa taarifa hii ya uchambuzi unalenga kutoa sababu za wanafunzi kufanya vizuri, wastani au vibaya katika upimaji huu. Taarifa inaonesha baadhi ya sababu zilizowafanya kupata alama za juu kama vile kuelewa matakwa ya swalii, kuwa na maarifa/ujuzi katika kuelezea dhana mbalimbali na kuwa na uelewa wa mada mbalimbali zilizopimwa. Aidha, sababu za wanafunzi kupata alama za wastani zimechangiwa na utoaji wa majibu yasiyojitosheleza. Hata hivyo, taarifa hii inaonesha pia sababu zilizofanya wanafunzi kufanya vibaya maswali ikiwa ni pamoja na kukosa maarifa/ujuzi katika kujieleza kwa ufasaha kuhusu dhana mbalimbali zinazohusiana na somo la Kiswahili.

Mrejesho huu utawawezesha wadau wa elimu, walimu na wanafunzi kupata mbinu muafaka katika kuboresha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika zoezi la upimaji wa Kidato cha Pili linaloendeshwa na Baraza la Mitihani la Tanzania.

Mwisho Baraza la Mitihani la Tanzania linatoa shukrani kwa Maafisa Mitihani, wataalam wa TEHAMA walimu na wadau wengine wa elimu waliohusika katika kutayarisha taarifa hii.



Dkt. Charles E. Msonde
KATIBU MTENDAJI

1.0 UTANGULIZI

Upimaji wa somo la Kiswahili kwa wanafunzi wa Kidato cha Pili ulifanyika Novemba 2019 na ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili kwa Kidato cha I na II. Upimaji huo ulikuwa na maswali 10 yaliyogawanyika katika sehemu A, B, C, D na E kwa kuzingatia mada za *Ufahamu, Sarufi, Uundaji wa Maneno, Aina za Maneno, Matumizi ya Lugha katika Miktadha mbalimbali, Fasihi kwa Ujumla na Uandishi wa Insha*. Wanafunzi walitakiwa kujibu maswali yote katika sehemu zote.

Taarifa hii inachambua viwango vya kufaulu vya wanafunzi wa Kidato cha Pili katika upimaji wa somo la Kiswahili (FTNA) 2019. Jumla ya wanafunzi **571,116** walipimwa katika somo la Kiswahili kwa mwaka 2019. Kati yao, wanafunzi **526,100** sawa na asilimia **92.19** ya wanafunzi wote walipimwa walifaulu kwa kupata daraja A hadi D. Kiwango hicho cha ufaulu kwa ujumla ni cha juu kwa asilimia **4.64** ikilinganishwa na ilivyokuwa mwaka 2018 ambapo, asilimia **87.55** ya wanafunzi walifaulu kwa kupata daraja A hadi D.

Uchambuzi huu umezingatia viwango vitatu vya kufaulu ambavyo ni *kiwango kizuri, wastani na hafifu*. Kiwango cha juu kilikuwa na alama 65 hadi 100 na kiliwakilishwa kwa rangi ya kijani, kiwango cha wastani kilikuwa na alama 30 hadi 64 na kiliwakilishwa kwa rangi ya njano na kiwango hafifu kilikuwa na alama 0 hadi 29 na kiliwakilishwa kwa rangi nyekundu. Hata hivyo, sampuli za majibu ya wanafunzi zimeambatanishwa ili kuonesha kilichotarajiwa kufanywa na kile kilichofanywa na wanafunzi.

Baraza la Mitihani la Tanzania linatarajia kuwa, uchambuzi huu utaimarisha ufundishaji na ujifunzaji wa somo la Kiswahili kwa walimu, wanafunzi na wadau wengine wa elimu katika kuweka mikakati ya kukuza na kuongeza viwango vya kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiswahili kwa vizazi vijavyo.

2.0 TATHMINI YA KILA SWALI

Sehemu hii inafafanua kwa kina uchambuzi wa kila swali na majibu yaliyotolewa na wanafunzi kwa kuonesha maswali yaliyojibiwa vizuri, wastani na yale yaliyojibiwa vibaya. Aidha, sababu za viwango mbalimbali vya kufaulu yaani kiwango cha juu, wastani na hafifu zimeelezwa bayana kwa kila swali. Sambamba na hayo, sampuli za majibu ya wanafunzi kwa kila swali zimeambatanishwa ili kuthibitisha maelezo ya uchambuzi huo.

2.1 SEHEMU A: UFAHAMU NA UFUPISHO

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mwanafunzi kuonesha umahiri katika kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali kisha kufupisha habari hiyo. Kifuatacho ni kifungu cha habari walichopewa:

*Katika miji mikubwa nchini Tanzania wimbi la ongezeko la watu bado ni kubwa. Ongezeko hilo la watu limesababisha kuzuka kwa matatizo makubwa maeneo ya mijini ikiwemo **msongamano** mkubwa wa magari na watu. Hali hii imesababisha wafanyakazi kuchelewa kazini, wanafunzi kuchelewa shulenii na hata wagonjwa kuchelewa kufikishwa katika vituo vya kutolea huduma za matibabu.*

*Hebu tuijulize, kwa nini watu wengi wanaondoka vijiji ni na kukimbilia mijini? Majibu yanaweza kuwa mengi, lakini miongoni mwa majibu hayo inaweza ikawa huduma zisizokidhi mahitaji ya kijamii. Jamii inatarajia kupata huduma bora za maji, umeme, barabara, matibabu, ajira na mawasiliano. Jamii inaposhindwa kupata huduma hizo katika **maskani** yao, lazima itafute huduma hizo nje. Na njia pekee ni kukimbilia mijini ambako huduma hizo zinapatikana.*

Anasa pia ni sababu mojawapo. Ikumbukwe kuwa kundi kubwa la watu wanaokimbilia mijini ni vijana. Kundi hili ni la watu wanaopenda starehe, hawataki kujituma na kujikwamua kimaisha, wanapenda kupata mafanikio ya haraka. Vijana wengi wanakimbilia mijini jambo ambalo linaleta wasiwasi wa hali ya maisha katika maeneo hayo ikilinganishwa na rasilimali zilizopo.

Wengi wao hujiingiza katika vitendo vya uhalifu kama wizi na utumiaji wa madawa ya kulevya.


*Ongezeko la watu mijini husababisha makazi duni, uchafuzi wa mazingira na uhalifu wa kila aina. Ongezeko la watu katika maeneo ya miji linakwenda sambamba na ongezeko la magari, hivyo tatizo la **miundombinu** isiyokidhi pia hujitokeza. Hali hii ikiachwa iendelee, uharibifu wa mazingira utaongezeka kwa kiasi kikubwa kwa sababu watu watatafuta njia mbadala ili kuzitatua **changamoto** zinazowakabili.*

2.1.1 Swali la 1: Ufahamu

Swali lilihusu *Ufahamu* na lilimtaka mwanafunzi kusoma kifungu cha habari kisha kujibu maswali yaliyofuata. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa ufahamu katika kusoma kifungu cha habari na kujibu maswali yanayotokana na kifungu hicho. Swali liligawanyika katika vipengele (a) hadi (d) na likuwa na jumla ya alama 9.

Vipengele (a) (i) hadi (iv) vilimtaka mwanafunzi kueleza maana ya maneno kama yalivyotumika katika kifungu cha habari. Kipengele (b) kilimtaka mwanafunzi (i) kutaja kundi la watu ambao hukimbilia mijini na (ii) kutaja sababu mbili muhimu zinazowafanya watu kukimbilia mijini. Kipengele (c) kilimtaka mwanafunzi kueleza iwapo ongezeko la watu mijini lisipodhibitiwa litasababisha nini na kipengele (d) mwanafunzi alitakiwa kupendekeza kichwa cha habari kisichozidi maneno matano kinachofaa kwa kifungu cha habari alichokisoma.

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 570,937 (100%) waliofanya upimaji na likuwa mionganoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 91.5 walifaalu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 1 inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.



Chati Na. 1: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 1

Chati Na. 1 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ambapo, wanafunzi 188,409 (33.0%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 5.5, wanafunzi 333,998 (58.5%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6 hadi 9 na wanafunzi 48,530 (8.5%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5.

Asilimia 58.5 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kuwa walielewa vyema kifungu cha habari na kuweza kujibu vipengele vingi kwa usahihi. Katika kipengele (a) (i) hadi (iv) waliweza kueleza maana za maneno kama *yalivyotumika* katika kifungu cha habari walichopewa kama *msongamano*; hali ya watu /magari kubanana, *maskani*; mahali anapoishi mtu/makazi/makao, *miundo mbinu*; barabara na *changamoto* ni matatizo. Kipengele (b) (i) waliweza kutaja vijana kuwa ni kundi la watu ambao hukimbilia mijini (ii) waliweza kutaja sababu mbili muhimu zinazowafanya watu wakimbilie mijini kama vile *huduma mbovu za kijamii vijijini*, *anasa na starehe*. Kipengele (c) waliweza kueleza kuwa, ongezeko la watu mijini lisipodhibitiwa kitu kitakachotokea ni *uharibifu wa mazingira kuongezeka kwa kiasi kikubwa* na katika kipengele (d) waliweza kupendekeza kichwa cha habari kinachofaa kuwa ni ONGEZEKO LA WATU MIJINI au

TATIZO LA MIUNDOMBINU. Kielelezo 1.1 ni majibu ya mwanafunzi aliyejibu vipengele (a), (b), (c) na (d) kwa usahihi.

Maswali

(a) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyotumika katika kifungu hiki cha habari.

(i) Msongamano...ni...hali...ya...kuwepo...kwa...watu...au...vitu...
kwa...wingi...sehemu...moja...au...ni...hali...ya...
kujazana...kwa...watu...sehemu...moja...

(ii) Maskani...ni...sehemu...ambapo...mtu...huishi...na...hufanya
shuhuti zake za kila siku.

(iii) Miundombinu...ni...vitu...au...huduma...zinazorahisisha...au...
zinazowezeshaa...maendeleo...ya...jamii...na...utendekeji...
wa...shughuli...za...kiachumi...Mtano...wa...miundombinu...
ni...barabara...

(iv) Changamoto...ni...matatizo...au...yikwazo...vinavyozua...
maendeleo...ya...jamii...au...watu...

(b) (i) Kulingana na kifungu cha habari ulichosoma ni kundi gani la watu hukimbilia mijini?
Kundi...kubwa...la...watu...wanokimbilia...mijini...
ni...vijana...

(ii) Taja sababu mbili muhimu zinazowafanya watu wakimbilie mijini.

- Kutokupata...huduma...zinazokidhi...mahitaji...
ya...kijamil...
- Kufuata...anasa...au...starehe...

(c) Ongezeko la watu mijini lisipodhibitiwa litasababisha nipi?

Ongezeko...la...watu...mijini...hwababisha...mokazi...duni...
uchafuzi...wa...mazingira...na...ubalifu...wa...kila...
qina...na...kuwepo...kwa...tatizo...la...miundombinu...uiye...
kidhi...

(d) Pendekeza kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu cha habari ulichosoma
kisichozi maneno matano.

.....ONGEZEKO...LA...WATU...MIJINI.....

Kielelezo 1.1: *Sampuli ya majibu sahihi ya mwanafunzi
katika swali la 1*

Kielelezo 1.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyelezea kwa usahihi maana za maneno *msongamano*, *maskani*, *miundombinu* na *changamoto* yaliyokuwa katika kipengele (a) (i) hadi (iv). Aidha, mwanafunzi huyo aliweza kutaja kundi la watu linalokimbilia mijini na sababu zinazowafanya kukimbilia mijini. Pia aliweza kutaja athari itakayotokea iwapo ongezeko la watu mijini halitadhibitiwa. Vivyo hivyo, mwanafunzi huyo alipendekeza kwa usahihi kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu cha habari alichopewa hivyo kupata alama zote za swali hili.

Wanafunzi wengine (33.0%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kutohana na kujibu kwa usahihi baadhi ya vipengele na kutoa majibu yasiyo jitoshela kwa vipengele vingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa majibu yasiyo sahihi katika kipengele (a) (iii) ambapo alitoa maana ya neno 'miundombinu' kuwa ni *kitu au kifaa maalumu.....* badala ya *barabara* kama lilivyotumika katika kifungu cha habari. Katika kipengele (iv) alilieleza neno 'changamoto' kuwa *ni hali ya kitu au vitu.....* badala ya *matatizo* na kipengele (b) (ii) alitaja sababu mojawapo inayowafanya watu wakimbilia mijini kuwa ni *ajira na mawasiliano*, badala ya *huduma mbovu za kijamii/anasa/starehe zilizoainishwa* katika kifungu cha habari. Kielelezo 1.2 kinaonesha sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu kwa usahihi vipengele (a) (iii), (iv) na (b) (ii) vyat swali hili.

- (iii) Miundombinu... Ni kitu au kifao... maalumtu... kilicho... tengenezwa..... na watu au nitu ili kitu mike na watu wengi ne.
- (iv) Changamoto... Ni bali ya kitu au vitu kujitokeza... katika kitu hicho
- (b)(ii) Taja sababu mbili muhimu zinazowafanya watu wakimbilia mijini.
- ...haduma... zisizokidhi... mahitaji... ya kijamii...
 - ...Ajira... na... mawasiliano...

Kielelezo 1.2: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyojitosheleza katika swali la 1*

Kielelezo 1.2 kinaonesha sehemu ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kueleza maana za maneno (iii) *miundombinu* na (iv) *changamoto*. Aidha, mwanafunzi huyo alishindwa kutaja sababu ya pili inayofanya watu kukimbilia mijini na hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi wachache (8.5%) walishindwa kujibu vipengele vingi vya swali hili na kupata alama hafifu. Kwa kiasi kikubwa, wanafunzi hao walionesha kutoelewa barabara kifungu cha habari walichopewa na hivyo kutoa majibu yasiyowiana na kifungu cha habari. Kielelezo 1.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepata alama hafifu katika swali hili.

Maswali

- (a) Eleza maana ya maneno yafuatayo kama yalivyonumika katika kifungu hiki cha habari.
- Msongamano... *Hali hii mesababisha wafanyakari kuchelewa karini wanafunzi huchelewa shulen ni na hata wagonjwa kuchelewa kufiki shwa kufikisituo yoka tolewa huduma za matibabu.*
 - Maskani... *Yao latu ma itafutwe huduma nje na njia pekee ni kuhimbilia mijini amba kote huduma hizi zinapatikana.*
 - Miundombinu... *Hali hii thi cithwa sendelec ahari bifu wamarangira utaongereza kwa jecesi kikubwa kwasababu watu wakata futa njia mbadala ili kuritatu.*
 - Changamoto... *Hali hii thi cithwa sendelec uharibifu wamarangira utaongereza kwa krasiti kikubwa kwasababu watu wa taufuna njia mbadala ili kuritatu zinazowakabili.*
- (b)
- Kulingana na kifungu cha habari ulichosoma ni kundi gani la watu hukimbia mijini? *kuneli hili ni lawatu wana upenda s丈che hawatati kujituma na kujitwa mua kimarango wanagendalatupata mafanikio haraka*
 - Taja sababu mbili muhimu zinazowafanya watu wakimbilie mijini.
 - *jemri inahitaji kupata huduma borara maji, umeme, barabara matibabu, ujira na mawasiliano*
 - *lakini miongoni una maji ba inayo inaweza ikawa huduma zis rokediti mahitaji ya cikrigamii*
- (c) Ongezeko la watu mijini lisipodhibiti litasababisha nini? *husababisha matazi dunia, kuchafuji wa marangira na uhalifu wakila dingi*
- (d) Pendekesa kichwa cha habari kinachofaa kwa kifungu cha habari ulichosoma kisichozidi maneno matano. *Anasa pia ni Sababu mojawapo.*


Kielelezo 1.3: Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi katika swali la 1

Kielelezo 1.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kutoa maana za maneno katika kipengele (a) (i) hadi (iv). Aidha, aliweza kutaja athari itakayotokea iwapo ongezeko la watu mijini halitadhibitiwa japokuwa hoja hiyo haikujitosheleza hivyo kupata alama hafifu.

2.1.2 Swali la 2: Ufupisho

Swali lilitoka katika mada ya *Ufahamu* na lililenga kupima umahiri wa wanafunzi katika kusoma na kuelewa habari kisha kuifupisha bila kuathiri maana iliyokusudiwa. Swali liliwa na jumla ya alama 6 na lilimtaka wanafunzi kufupisha habari aliyoysoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60).

Swali hili lilijibiwa na wanafunzi 560,722 sawa na asilimia 98.2 ya wote waliofanya upimaji. Swali hili liliwa mionganoni mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 77.5 ya wanafunzi hao walifaalu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 2 inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.



Chati Na. 2: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 2

Chati Na. 2 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ambapo, wanafunzi 308,958 (55.1%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 3.5, wanafunzi 125,602 (22.4%) walifaalu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 4 hadi 6 na wanafunzi 126,162 (22.5%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 1.5.

Kati yao, nusu ya wanafunzi wote waliojibu swali hili (55.1%) walifaalu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 2 hadi 3.5. Majibu ya wanafunzi hao yalionesha

kutojitosheleza kwa baadhi ya mambo muhimu katika uandishi wa ufupisho. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika ufupisho wenyewe idadi kubwa ya maneno yaani maneno 77 na hakueleza sababu za watu wengi kukimbilia mijini. Aidha, alitumia maneno yasiyo sanifu kwa baadhi ya hoja alizotoa. Pia, mwanafunzi huyo aliandika ufupisho kwaaya mbili tofauti kinyume na kanuni/taratibu za ufupishozinazotakiwa kuzingatiwa yaani kutumia aya moja pekee. Kielelezo 2.1 ni jibu la mwanafunzi aliyeandika ufupishousiojitosheleza na kupata alama za wastani.

2. Andika ufupisho wa kifungu cha habari ulichosoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60).

Ongezeko la watu katika mijini mikubwa nchini kivetu imetuwa kubwa sana. Iw sababu ya Ongezeko hito kumezuka matatizo makubwa katika mijini mikubwa kama Dar-es-salam, Mwanza na Arusha. Matatizo hayo ni kama msongamano mikubwa wa magari na watu ambayo hali hii imesahabisha waifanyikazi kuchelewa kazini wanafunzi kuchelewa mashulen na hata pia watu kuchelewa masafarini au wagenjwa kuchelewa hospitalini. Watu wengi huondoka vijini kuao na kukimbilia mijini ili kupata huduma bora za maji, umeme, barakara, matibabu, ajira na mawasiliano.

Kielelezo 2.1: Sampuli ya jibu la mwanafunzi lisilojitosheleza

Kielelezo 2.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeandika ufupisho wenyewe idadi kubwa ya maneno, pia hakueleza sababu za watu wengi kukimbilia mijini. Halikadhalika, alitumia maneno yasiyo sanifu kama vile *mashulen* na *masafarini* na hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, asilimia 22.4 ya wanafunzi waliojibu swalihili walifaulu vizuri kwa kupata alama za juu kuanzia 4 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kutumia maarifa stahiki katikakufupisha habari kwa kuzingatia taratibu zote za uandishi wa

ufupisho kama vile; *mpango wa mawazo wenyewe mantiki, matumizi ya alama na vituo, kutumia maneno yao wenyewe bila kupotosha kiini cha habari, idadi ya maneno na matumizi ya lugha sanifu*. Kielelezo 2.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyefupisha habari kwa kuzingatia mambo muhimu na kupata alama za juu.

2. Andika ufupisho wa kifungu cha habari ulichosoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60)

Kumekuura na winyi la ongezeko kubwa la watu mijini. Hii ni kutokana na hali ya maisha yaliyoko kijinini ambapo watu hushindwa kupata huduma zinazokidhi mahitaji ya jamii. Inauzemekana kuwa watu wanadorezeza kua wingi ni vijana. Vijana huperenda utandhe na hitaka kupata mafanikie ya haraka kua hiyo vijana hawa huja mijini kua sababu ya anasa. Hili jumbo huleta usarivasi wa hali ya maisha katika maneno hayo. Ongezeko la watu hushindwa uchafuri wa mazingira na ubaliyu wa kila aina. (maneno 60)

Kielelezo 2.2: *Mwanafunzi aliyejibu vizuri swali la 2*

Kielelezo 2.2 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyefupisha habari kwa kuzingatia taratibu zote za uandishi wa ufupisho hususan kutumia maneno yake mwenyewe bila kupotosha kiini cha habari, kuwa na mtiririko wenyewe mantiki na idadi sahihi ya maneno na hivyo kupata alama zote.

Licha ya swali hili kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, asilimia 22.5 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 1.5. Wanafunzi hao walishindwa kuzingatia taratibu za uandishi wa ufupisho wa habari. Baadhi yao waliandika habari ndefu na zisizozingatia mawazo makuu yaliyo katika habari kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika habari yenyе maneno (160) inayohusu watu kukimbilia mijini na kuacha watoto wachanga wakiteseka bila uangalizi na kuelezea madhara ya kufanya kazi katika umri mdogo; mawazo ambayo hayakuwa katika kifungu cha habari. Kielelezo 2.3 kinaonesha sampuli

ya jibu la mwanafunzi aliyefupisha habari bila kuzingatia taratibu za uandishi wa ufupisho na kupata alama hafifu.

2. Andika ufupisho wa kifungu cha habari ulichosoma kwa maneno yasiyopungua hamsini (50) na yasiyozidi sitini (60).
- Katika miji mikubwa t Tanzania watu wamekuwa waki kimbia mijini na na kusabashisha ogezeko. Ie watu kuwa wengi. Kuamana hiyo watu wakionta marsha magumu anaamua kukiimbili id mijini mwiningine ana amua kukiimbida yeye kama yeye wendae alikuwa ana familia yake anaachia watoto vijini yeye anendela mijini humu atatembea atazurela na baadie atatafaa mtu mwiningine ate mzalishia watoto wengine wale ameswateketea vijini huko. Haku tujaribii kuwa watu wema namna hiyo tina acha watoto wedogo kabisa hawawesi kujitegemea tatizo hili limesababisha kuruka kua matatizo mbalimbali ya kifamilia katika nchi ya Tanzania tumekuwa na tabia kama hiyo unapo onloka kijini unajua una batoto aneye nyo nya unamwachia nani autumzie wakati unajua kabisa kiumbe chaka kima nyanya bba nengachia nacho sige una muacha mtoto harafu we we unendela mijini ceta pata matutizo mengi na baadie atakufa. Kuahiyu tunashio jifunza hapa tusikimbile mijini tulicija wakito tusikimbile mijini Kifanyi kasi tutiwa na umri chini ya miko "18" tuti pata magonjwa na baadie nassisi tuti kupa. Ongereke launtu mijini pia husababishwa na uchafizi warazingira na uhalifu wa kili aina yaani witi. Sambamba na ongerereko la magari msangi maria uod Magari. Urekeko mudogaji.

Kielelezo 2.3: Sampuli ya jibu la mwanafunzi lisilozingatia vigezo vyote vyaya ufupisho

Kielelezo 2.3 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeandika habari isiyokidhi taratibu yoyote ya uandishi wa ufupisho hususan kutumia maneno yenye kupotosha kiini cha habari na kutokuwa na mtiririko wenye mantiki, pia alitumia idadi kubwa ya maneno na hivyo kupata alama hafifu.


2.2 SEHEMU B: SARUFI

Sehemu hii ilihu sarufi na ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mwanafunzi kutumia maarifa mahususi kuhusu maumbo na maana mbalimbali za maneno katika lugha ya Kiswahili.

2.2.1 Swali la 3: Uundaji wa Maneno

Swali hili lilitoka katika mada ya *Uundaji wa Maneno* na mada ndogo ya *Kutumia Uambishaji*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi katika uundaji wa maneno ya Kiswahili. Swali lilimtaka mwanafunzi kubainisha mzizi wa asili wa kila kitenzi katika sentensi alizopewa na ilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 99.3 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji na ilikuwa mionganini mwa maswali yaliyojibiwa vizuri ambapo asilimia 66.1 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 3 inaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu kwa asilimia.



Chati Na. 3: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 3

Chati Na. 3 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ambapo, wanafunzi 302,755 (53.4%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6, wanafunzi 192,198 (33.9%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5 na wanafunzi 72,003 (12.7%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10.

Zaidi ya nusu ya wanafunzi (53.5%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu chenyе alama kuanzia 3 hadi 6. Wanafunzi hao waliweza kubainisha mzizi wa asili wa kitenzi kwa baadhi ya sentensi kwa usahihi na kushindwa katika sentensi nyingine. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alishindwa kubainisha kwa usahihi mzizi wa asili wa kitenzi katika kipengele (e) viliharibiwa kwa kuandika ‘rib’ badala ya ‘harib’, (f) alitambulisha; *lish* badala ya ‘tambu’, (h) alimuonesha; *nesh* badala ya ‘on’, (i) walipokelewa; *pok* badala ya ‘poke’ na (j) walitolewa; *lew* badala ya ‘to’. Aidha, mwanafunzi huyo alibainisha kwa usahihi mzizi wa kitenzi katika kipengele a, b, c, d na g. Kielelezo 3.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyojitosheleza katika swali hili.

3. Bainisha mzizi wa asili wa kila kitenzi katika sentensi zifuatazo:

- (a) Mtoto anacheza mpira.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni chez
- (b) Wanafunzi wanapigana darasani.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni pig
- (c) Sisi hatupendani.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni Pend
- (d) Watoto walifungiana milango.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni fung
- (e) Vifaa feki viliharibiwa.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni rib
- (f) Mwalimu alitamblyisha wanafunzi wageni.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni lish.
- (g) Jana hatukusomeana.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni som
- (h) Mama alimuonesha baba daftari langu.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni nash
- (i) Mamia ya wachezaji wa Taifa Stars walipokelewa kwa shangwe.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni Pok
- (j) Wakorofsi walitolewa darasani.
Mzizi wa kitenzi katika sentensi hii ni lew

Kielelezo 3.1: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepeata alama za wastani*

Kielelezo 3.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeeweza kubainisha mzizi wa kitenzi katika sentensi a, b, c, d na g ; huku akishindwa katika sentensi e, f, h, i na j, hivyo kupata alama za wastani.

Wanafunzi wachache (12.7%) walijibu swali hili vizuri na kupata alama za juu yaani 6.5 hadi 10 kutokana na kuwa na uelewa mkubwa kuhusu dhana ya mzizi katika vitenzi vya Kiswahili. Wanafunzi hao waliweza kubainisha kwa usahihi

mzizi wa kitenzi katika sentensi zote walizopewa kama vile: (a) anacheza - ‘chez’, (b) wanapigana - ‘pig’, (c) hatupendani - ‘pend’, (d) walifungiana - ‘fung’, (e) viliharibiwa - ‘harib’, (f) alitambulisha - ‘tambu’, (g) hatukusomeana - ‘som’, (h) alimuonesha - ‘on’, (i) walipokelewa - ‘poke’ na (j) walitolewa - ‘to’. Kielelezo 3.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili.

3. Bainisha mzizi wa asili wa kila kitenzi katika sentensi zifuatazo:

- (a) Mtoto anacheza mpira.
Mzizi wa asili wa kitenzi anacheza ni "chez"
- (b) Wanafunzi wanapigana darasani.
Mzizi wa asili wa kitenzi wanapigana ni "pig"
- (c) Sisi hatupendani.
Mzizi wa asili wa kitenzi hatupendani ni "pend"
- (d) Watoto walifungiana milango.
Mzizi wa asili wa kitenzi walifungiana ni "fung"
- (e) Vifaa feki viliharibiwa.
Mzizi wa asili wa kitenzi viliharibiwa ni "harib"
- (f) Mwalimu alitambulisha wanafunzi wageni.
Mzizi wa asili wa kitenzi alitambulisha ni "tambu"
- (g) Jana hatukusomeana.
Mzizi wa asili wa kitenzi hatukusomeana ni "som"
- (h) Mama alimuonesha baba daftari langu.
Mzizi wa asili wa kitenzi alimuonesha ni "on"
- (i) Mamia ya wachezaji wa Taifa Stars walipokelewa kwa shangwe.
Mzizi wa asili wa kitenzi walipokelewa ni "poke"
- (j) Wakorofu walitolewa darasani.
Mzizi wa asili wa kitenzi walitolewa ni "to"

Kielelezo 3.2: *Sampuli ya jibu sahihi la mwanafunzi katika swali la 3*

Kielelezo 3.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyebainisha kwa usahihi mzizi wa asili wa kitenzi katika vitenzi vilivyo katika sentensi (a) hadi (j).

Licha ya swali hilo kuwa na kiwango kizuri cha kufaulu, asilimia 33.9 ya wanafunzi waliojibu swali hili walipata alama hafifu kuanzia 0 hadi 2.5 kutokana na kuwa na uelewa mdogo kuhusu mzizi wa asili wa vitenzi. Miongoni mwao, asilimia 22.4 walishindwa kabisa kubainisha mzizi wa asili wa kitenzi katika sentensi zote na kupata 0. Baadhi yao walionesha kutoelewa dhana ya mzizi wa asili katika kitenzi, hivyo walieleza kazi za viambishi mbalimbali katika sentensi husika na wengine walibainisha aina za maneno katika sentensi hizo na kueleza maana ya misamiati (vitenzi) katika sentensi hizo. Kielelezo 3.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili.

3. Bainisha mzizi wa asili wa kila kitenzi katika sentensi zifuatazo:

- (a) Mtoto anacheza mpira.
.....
.....
- (b) Wanafunzi wanapigana darasani.
.....
.....
- (c) Sisi hatupendani.
.....
.....
- (d) Watoto walifungiana milango.
.....
.....
- (e) Vifaa feki viliharibiwa.
.....
.....
- (f) Mwalimu alitambulisha wanafunzi wageni.
.....
.....
- (g) Jana hatukusomeana.
.....
.....
- (h) Mama alimuonesha baba daftari langu.
.....
.....
- (i) Mamia ya wachezaji wa Taifa Stars walipokelewa kwa shangwe.
.....
.....
- (j) Wakorofu walitolewa darasani.
.....
.....

Kielelezo 3.3: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeputa alama hafifu*

Kielelezo 3.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyebainisha aina za vitenzi katika vipengele (a), (b), (d), (f), (h) na (i). Pia alibainisha dhima za viambishi katika vitenzi kwa vipengele (c), (g) na (j) na katika kipengele (e), alibaini neno 'feki' kuwa ni kitenzi badala ya *viliharibiwa*.

2.2.2 Swali la 4: Aina za Maneno

Swali lilitoka katika mada ya *Aina za maneno* katika mada ndogo ya *Ufafanuzi wa Aina Saba za Maneno na Matumizi ya Kamusi*. Swali lililenga kupima maarifa na lilikuwa na jumla ya alama 10. Swali hili lilikuwa na vipengele viwili vilivyomtaka mwanafunzi (a) kueleza maana ya maneno mbalimbali na (b) kubainisha aina za nomino alizopewa.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 99.8 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji na lilikuwa mionganini mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu. Asilimia 60.1 ya wanafunzi waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 1 linaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.

Jedwali Na. 1: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya Wanafunzi
0.0 - 2.5	227,478	39.9
3.0 - 6.0	243,441	42.7
6.5 - 10	99,200	17.4

Jedwali Na. 1 linaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ambapo wanafunzi 243,441 (42.7%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6, wanafunzi 99,200 (17.4%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10 na wanafunzi 227,478 (39.9%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5.

Wanafunzi 243,441 sawa na asilimia 42.7 waliofaulu kwa kiwango cha wastani, walieleza kwa usahihi baadhi ya vipengele vya sarufi walivyopewa na kushindwa katika vipengele vingine. Wanafunzi hao walitoa maana za misamiati zisizojitosheleza katika kipengele (a) na kuchanganya baadhi ya aina za nomino katika kipengele (b). Kielelezo 4.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeweza kubainisha aina za nomino katika kipengele (b) na kushindwa kueleza maana

za maneno kwa baadhi ya vipengele katika (a) na kupata alama za wastani.

4. (a) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

- (i) Kidahizo
Ni...mkazo...wa...neno./ni...pale...ambapo...ntumiaji...
wa...lugh...anaweka...mka...katika...neno.....
- (ii) Kitomeo
Ni...kitua...ambasha...hutumika...katika...ubeti...
wa...ushairi./ni...mwisha...wa...tungo...ya...beti...
mfano...usiku...wa...mbalamuzi...wakoto...hufurashia...
- (iii) Alfabeti
Ni...mpangilia...wa...herufi...katika...mwenendo...
wa...kuanzia...mwanzo...hadi...mwisho...
- (iv) Kamusi
Ni...kitabu...chenye...orodha...ya...maneno...yalijopangwa
kwa...alfabeti...pamoja...na...maana...zake...
- (v) Kitenzi
Ni...nena...ambalo...linasimama...kama...lenye...
...ni...kuuera...kusaidia...sentensi...kwa...namna...
moja...au...nyingine...

(b) Bainisha aina ya nomino zifuatazo:

Mfano: Maji – nomino ya jumla/wingi

- (i) Papai.Nomino...ya...kawaida.....
- (ii) Mungu.Nomino...dhahania.....
- (iii) Arusha.Nomino.....ya...pekee.....
- (iv) Upopo.Nomino...dhahania.....
- (v) Jumamosi.Nomino...ya...pekee.....

Kielelezo 4.1: *Sampuli ya majibu ya swali la 4 yasiyojitosheleza*

Kielelezo 4.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kueleza maana za maneno katika kipengele (a) kwa kuelezea (i) Kidahizo - *mkazo katika neno* badala ya maneno yaliyokolezwa wino katika kamusi, (ii) Kitomeo - *kituo katika ubeti wa ushairi* badala ya kidahizo pamoja na maelezo/maana yake yote na (v) Kitenzi - *neno ambalo*

linasimama kama lenyewe ili kuweza kusaidia sentensi badala ya maneno ambayo huongelea kuhusu matendo yali/yata/yanayotokea. Aidha, mwanafunzi huyo alibainisha aina za nomino katika kipengele (b) (i) hadi (v) kwa usahihi na kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi 227,478 sawa na asilimia 39.9 waliokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu walishindwa kueleza maana ya maneno katika kipengele (a) na kushindwa kubainisha aina za nomino katika kipengele (b). Hii ilitokana na wanafunzi hao kuwa na uelewa mdogo kuhusu maana za misamiati mbalimbali na aina za nomino. Kwa mfano, katika kipengele (a), baadhi ya wanafunzi walichanganya maana za dhana za kamusi walizopewa na aina za nomino zilizo katika kipengele (b). Kielelezo 4.2 ni sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya swalii hili.

4. (a) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

(i) Kidahizo
*Ni.....maandishi.....ktk.....sentensi.....ambayo.....
hwa.....na.....rang'i.....ya.....mkolezo!*

(ii) Kitomeo
Ni.....maneno.....yote.....ktk.....sentensi!

(iii) Alfabeti
*Ni.....henyi.....sa.....maneno.....sina.....organista.....
sentensi.....tafauti!*

(iv) Kamusi
*Ni.....kitabu.....cha.....marejia.....yepye.....misamati.....
iliyokusanya.....ktk.....jamii.....tafauti.....za.....
wafu!*

(v) Kitepzzi
*Ni.....maneno.....yanayooresha.....zaudi.....
kuhusu.....nomino!*

(b) Bainisha aina ya nomino zifuatazo:

Mfano: Maji – nomino ya jumla/wingi

(i) Papai. *Nomino.....dhahania!*
(ii) Mungu. *Nomino.....ya.....kipetee,*
(iii) Arusha. *Nomino.....ya.....mahali!*
(iv) Upendo. *Nomino.....ya.....kipetee*
(v) Jumamosi. *Nomino.....ya.....Jumla!*

Kielelezo 4.2: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama hafifu

Kielelezo 4.2 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi ambaye katika kipengele (a) alishindwa kutoa maana za dhana zote na katika kipengele (b) alichanganya aina za nomino kwa baadhi ya vipengele na kupata alama za chini.

Wanafunzi wachache (99,200) sawa na asilimia 17.4 waliofaulu kwa kiwango cha juu walieleza kwa usahihi maana za maneno katika vipengele (a) (i) Kidahizo; *maneno yaliyokolezwa wino katika kamusi*, (ii) Kitomeo; *kidahizo*

pamoja na maelezo/maana yake yote, (iii) Alfabeti; herufi ambazo zipo katika mpangilio maalum zinazotumika kuunda maneno, (iv) Kamusi; kitabu chenye maneno yaliyopangwa kialfabeti pamoja na maana zake timilifu na (v) Kitenzi; maneno ambayo huongelea matendo yali/yata/yanayotokea. Wanafunzi hao pia waliweza kubainisha aina za nomino katika kipengele (b) (i) 'Papai' nomino ya kawaida, (ii) 'Mungu' nomino dhahania, (iii) 'Arusha' nomino ya pekee, (iv) 'Upopo' nomino dhahania na (v) 'Jumamosi' nomino ya pekee sawa kabisa na majibu yaliyotakiwa katika swali hili. Kielelezo 4.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu swali hili kwa usahihi.

4. (a) Eleza maana ya maneno yafuatayo:

- (i) Kidahizo
.....ni.....maneno.....yalijyo.....kolewa.....wino.....katika.....
.....kamusi:
.....
- (ii) Kitomeo
.....ni.....kidahizo.....pamoja.....na.....maelezo.....yake.....yote.....au.....maana.....
.....yake.....yote:
.....
- (iii) Alfabeti
.....ni.....herufi.....ambayo.....zipo.....katika.....mpangilio.....maalumu.....
.....hutumika.....kuunda.....maneo:
.....
- (iv) Kamusi
.....ni.....kitabu.....chonye.....maneno.....yalijye.....pangwa.....kifalabetti.....
.....pamoja.....na.....maana.....sake.....timiliyu:
.....
- (v) Kitenzi
.....ni.....maneno.....ambayo.....huongelea.....kubuee.....matendo.....yalijyotako.....
.....yatayotako.....na.....yanayteken:
.....

(b) Bainisha aina ya nomino zifuatazo:

Mfano: Maji – nomino ya jumla/wingi

- (i) Papai.....nomino.....ya.....kawaida.....
(ii) Mungu.....nomino.....chahania.....
(iii) Arusha.....nomino.....pekee.....
(iv) Upendo.....nomino.....ya.....chahania.....
(v) Jumamosi.....nomino.....pekee.....

Kielelezo 4.3 : *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri swali la 4*

Kielelezo 4.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeeleza maana ya misamiati (i) hadi (v) katika kipengele (a) na kubainisha aina za nomino katika kipengele (b) kwa usahihi.


2.3 SEHEMU C: MAWASILIANO NA UTUMIZI WA LUGHA

Sehemu hii ilikuwa na maswali mawili yaliyomtaka mwanafunzi kuonesha uwezo wa kutumia lugha katika miktadha mbalimbali na katika mawasiliano.

2.3.1 Swali la 5: Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na mada ndogo ya *Rejesta*. Swali lilengesa kupima matumizi na lilimtaka mwanafunzi kuonesha mazingira ambayo rejesta katika kipengele (a) hadi (e) hutumika na lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibowi na asilimia 99.4 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji na lilikuwa mionganini mwa maswali yaliyojibowi vizuri sana na wanafunzi wengi ambapo, asilimia 94.3 walifaulu kwa kiwango cha juu na cha wastani. Chati Na. 4 inaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu kwa asilimia.



Chati Na. 4: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 5

Chati Na. 4 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika swali hili ambapo, wanafunzi 296,451 (52.2%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10, wanafunzi 239,091 (42.1%) walifaulu kwa kiwango

cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na wanafunzi 32,371 (5.7%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5.

Zaidi ya nusu ya wanafunzi wote (52.2%) waliofaulu kwa kiwango kizuri walionesha kwa usahihi mazingira ambayo rejestu katika kipengele (a) hadi (e) hutumika kwa kuwa walikuwa na mawanda mapana kuhusu matumizi ya lugha katika mazingira tofauti tofauti. Hivyo, wanafunzi hao waliweza kubaini mazingira mbalimbali ambayo rejestu hizo hutumika kama vile (a) *Mimi kuku ugali moja, huyu wali maharage na wale pale ng'ombe* (Hotelini), (b) *Zuia babu, kula hivyo vichwa vitatu* (kwenye daladala), (c) *Napenda kujibu swali la nyongeza....* (Bungeni), (d) *Ndugu Madongo Kuinuka unatuhumiwa kwa kosa la jinai la* (Mahakamani) na (e) *Jipatie mahitaji ya jikoni; nyanya, vitunguu, karoti,* (Sokoni). Kielelezo 5.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri swali la 5.

5.	Onesha rejestu zifuatazo hutumika katika mazingira gani.
(a)	Mimi kuku ugali moja, huyu wali maharage na wale pale Ng'ombe. <i>Aina hii ya rejestu hutumika hotelini:</i>
(b)	Zuia babu, kula hivyo vichwa vitatu. <i>Aina hii ya rejestu hutumika bungeni:</i>
(c)	Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kama ifuatavyo. <i>Aina hii ya rejestu hutumika bungeni:</i>
(d)	Ndugu Madongo Kuinuka unatuhumiwa kwa kosa la jinai la kuiba mali ya umma. <i>Aina hii ya rejestu hutumika mahakamani:</i>
(e)	Jipatie mahitaji ya jikoni, nyanya, vitunguu, karoti, hoho, pilipili na ndimu vyote viro. <i>Aina hii ya rejestu hutumika sokoni:</i>

Kielelezo 5.1: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyeepata alama za juu*

Kielelezo 5.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyebeaini kwa usahihi mazingira yote ambayo rejestaa (a) hadi (e) hutumika na kupata alama zote.

Asilimia 42.1 ya wanafunzi waliofaulu kwa kiwango cha wastani walishindwa kuonesha kwa usahihi baadhi ya rejestaa walizopewa kuwa hutumika katika mazingira gani, hivyo kuwa na majibu yasiyojitosheleza na kupata alama za wastani. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliweza kuonesha kwa usahihi mazingira zinakotumika rejestaa za kipengele (a), (d) na (e) kwa kutoa majibu kama vile: (a) *rejestaa za hotelini*, (d) *rejestaa za mahakamani* na (e) *rejestaa za sokoni* lakini alishindwa kuonesha kwa usahihi mazingira ambayo rejestaa (b) na (c) hutumika kwa kuandika (b) *rejestaa za hotelini* badala ya 'kwenye daladala' na (c) *rejestaa za mkutano* badala ya 'bungeni' kama kielelezo 5.2 kinavyodhihirisha majibu ya mwanafunzi huyo katika swali hili.

5. Onesha rejestaa zifuatazo hutumika katika mazingira gani.

- (a) Mimi kuku ugali moja, huyu wali mjaharage na wale pale Ng'ombe.
.....*rejestaa za hotelini*.....
- (b) Zuia babu, kula hivyo vichwa vitatu.
.....*rejestaa za hotelini*.....
- (c) Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kama ifuatavyo.
.....*rejestaa za mkutano*.....
- (d) Ndugu Madongo Kuinuka unatuhumiwa kwa kosa la jinai la kuiba mali ya umma.
.....*rejestaa za mahakamani*.....
- (e) Jipaties mahitaji ya jikoni, nyanya, vitunguu, karoti, hoho, pilipili na ndimu vyote viro.
.....*rejestaa za Sokoni*.....

Kielelezo 5.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepeata alama za wastani*

Kielelezo 5.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyebeainisha kwa usahihi mazingira ya rejestaa zilizo katika vipengele (a),

(d) na (e) na kushindwa kubaini mazingira ya rejestra (b) na (c) na kupata alama za wastani.

Licha ya kiwango kizuri cha kufaulu, wanafunzi wachache (5.7%) waliojibu swali hili walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu kwa kupata alama za chini kuanzia 0 hadi 2.5. Wanafunzi hao hawakuwa na uelewa wa kutosha kuhusu dhana ya rejestra na hivyo kushindwa kubainisha mazingira zinakotumika rejestra walizopewa. Asilimia 2.8 ya wanafunzi hao walipata alama 0 kutokana na kutokuwa na maarifa yoyote kuhusu rejestra na hivyo baadhi yao walichanganya dhana ya rejestra na sifa za lugha, misimu na ama wahusika wa fasihi simulizi kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa majibu katika vipengele (a) hadi (e) kwa kuandika *sauti za nasibu, chombo cha mawasiliano, lugha zagao, watu na wanyama*; majibu ambayo hayana uhusiano wowote na rejestra alizopewa. Pia, wanafunzi wengine walishindwa kujibu swali hili kutokana na kutaja aina mbalimbali za rejestra kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 5.3 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili.

5. Onesha rejestra zifuatazo hutumika katika mazingira gani.

- (a) Mimi kuku ugali moja, huyu wali maharage na wale pale Ng'ombe.
Rejestra ya chahula.....
- (b) Zuiq babu, kula hivyo vichwa vitatu.
Rejestra ya nyumbani.....
- (c) Napenda kujibu swali la nyongeza la Mheshimiwa kama ifuatavyo.
Rejestra ya darascuni.....
- (d) Ndugu Madongo Kuinuka unatuhumiwa kwa kosa la jinai la kuiba mali ya umma.
Rejestra ya makomani.....
- (e) Jipatie mahitaji ya jikoni, nyanya, vitunguu, karoti, hoho, pilipili na ndimu vyote viro.
Rejestra ya viingo.....


Kielelezo 5.3: *Sampuli ya jibu baya la mwanafunzi katika swali la 5*

Kielelezo 5.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyetaja aina mbalimbali za rejestra kama vile (a) *Rejesta ya chakula*, (b) *Rejesta ya nyumbani*, (c) *Rejesta ya darasani* na (e) *Rejesta ya viungo* hivyo kupata alama hafifu.

2.3.2 Swali la 6: Lugha ya Mazungumzo

Swali lilitoka katika mada ya *Matumizi ya Lugha katika Miktadha Mbalimbali* na mada ndogo ya *Lugha ya Kimazungumzo na Kimaandishi* na lilengen kupima tathmini. Swali lilikuwa na jumla ya alama 10 na lilimtaka mwanafunzi kufafanua sifa tano za lugha ya kimazungumzo.

Swali hili lilijibwa na asilimia 97.8 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo asilimia 30.1 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 5 inaonesha viwango vya wanafunzi vya kufaulu kwa asilimia.



Chati Na. 5: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 6

Chati Na. 5 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi ambapo, wanafunzi 386,002 (69.1%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5, wanafunzi 145,239 (26%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia

3 hadi 6 na wanafunzi 27,372 (4.9%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10.

Wanafunzi wengi (69.1%), waliojibu swali hili waliokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu walikosa umahiri katika kutambua sifa za lugha ya mazungumzo na lugha ya maandishi. Miongoni mwao, asilimia 42.3 walipata 0 kutokana na kushindwa kabisa kufafanua sifa hata moja kuhusu lugha ya kimazungumzo. Baadhi ya wanafunzi walikabiliwa na tatizo la kuchanganya ‘lugha’ na ‘fasihi’, hivyo kuandika sifa za fasihi simulizi kama vile; *ni mali ya jamii, hurithishwa toka kizazi kimoja hadi kingine na huhifadhiwa kichwani*; majibu yasiyo sahihi kulingana na sifa za lugha ya mazungumzo. Wapo wanafunzi waliofanua dhima za fasihi kama vile; *kuelimisha jamii, kukuza lugha, kuhifadhi utamaduni, kufundisha maadili mema na kuonya jamii*. Wengine walifafanua dhima za lugha badala ya kufafanua sifa za lugha ya mazungumzo kama vile; (a) *huwa na mzungumzaji na msikilizaji*, (b) *Humkutanisha ana kwa ana mzungumzaji na msikilizaji*, (c) *Huonesha hali ya mzungumzaji kama hasira, huzuni, furaha*, (d) *Hutolewa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo na* (e) *huweza kubadilika kutokana na mazingira*. Kielelezo 6.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili.

6. Fafanua sifa tano za lugha ya kimazungumzo.

- (a) *Kuelimisha Jamii, Mazungumzo yanetlimusig Jamii na Taifa pia kue Ujumla zaidi kuna uruhu usto na Vijana pia.....*
- (b) *hukuza lugha Mazungumzo hilete nswa ya Kuenda kue heretka Jamii lugha kathika Jamii mbalimbali,*
- (c) *Huruthishwa mawasiliano, lugha ya mazungumzo huseidza kuwasiliana kwa heretka sandi na kilokoti muda pia.....*
- (d) *Hufundishi Utamaduni, Mazungumzo hilete ukizuri wa Utamaduni kathika Jamii na Taifa kue Ujumla*
- (e) *Hufundishi madili, mony, Mazungumzo hufundishi uruhu mastili mema, tabii njema, na Kuonya pia.....*

Kielelezo 6.1: Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya swali hili

Kielelezo 6.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyefafanua dhima za lugha kama *kurahisisha mawasiliano* na *lugha kama kitambulisho cha jamii* na dhima za fasihi kama *kuhifadhi utamaduni*, *kuelimisha jamii na kufundisha maadili* kinyume na matakwa ya swali, hivyo kupata alama hafifu.

Aidha, asilimia 26 ya wanafunzi waliokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu waliweza kufafanua kwa usahihi baadhi ya sifa za lugha ya mazungumzo na kushindwa sifa nyingine. Tatizo lililowakabili wanafunzi hawa kwa kiasi kikubwa ni kuchanganya lugha ya kimazungumzo na tofauti iliyopo kati ya fasihi andishi na fasihi simulizi. Kielelezo 6.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyepeata alama za wastani.

6. Fafanu sifa tano za lugha ya kimazungumzo.

- (a) *Huwasilishwa...kwa...njia...ya...mdomo...Lugha...ya...kimazungumzo...hua...hupitishwa...kwa...njia...ya...mdomo...kutoka...kwa...mtu...mmoja...kwenda...mwengime.....*
- (b) *Chanzo...chake...ni...msemaji...na...kikomo...chake...ni...msikilizaji...Lugha...ya...kimazungumzo...hutoka...kwa...msemaji...kwenda...kwa...msikilizaji.....*
- (c) *Haina...gharama...kwasobabu...mzungumzaji...hupiki...cho...taariyo...au...yumbi...kwa...njia...ya...mdomo.....*
- (d) *I-labori...ikolewayo...kua...lugha...ya...mazungumzo...hupikia...watu...wachache.....*
- (e) *Lugha...ya...mazungumzo...hua...ni...changamoto.....*

Kielelezo 6.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi lisilojitosheleza*

Kielelezo 6.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyefafanua sifa mbili sahihi za lugha ya kimazungumzo kama vile, (a) *huwasilishwa kwa njia ya mdomo*, (b) *chanzo chake ni msemaji na kikomo chake ni msikilizaji*. Pia, mwanafunzi huyo alishindwa kufafanua sifa za lugha ya kimazungumzo kwa

kuandika katika (c) *haina gharama*, (d) *habari itolewayo kwa lugha ya mazungumzo hufikia watu wachache na* (e) *lugha ya mazungumzo huwa ni changamano*; majibu ambayo ni kinyume na matakwa ya swalı.

Wanafunzi wachache (4.9%), waliofaulu kwa kiwango kizuri na kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10 waliweza kufafanua kwa usahihi sifa tano za lugha ya kimazungumzo kama vile: (a) *Ina mzungumzaji na msikilizaji*, (b) *Humkutanisha ana kwa ana mzungumzaji na msikilizaji*, (c) *Huonesha hali ya mzungumzaji kwa wakati huo kama hasira, huzuni, furaha*, (d) *Hutolewa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo na* (e) *Inaweza kubadilika kutokana na mazingira kama kielelezo 6.3 kinavyoonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi huyo.*

6. Fafanua sifa tano za lugha ya kimazungumzo.
- (a) *Ina mzungumzaji na msikilizaji. Yupo yule aneyo nta..... a. mazungumzo (mzungumzaji) na yule aneyesukali za msikilizaji).*
- (b) *Humkutanisha ana kwa ana yule mzungumzaji na msikilizaji.*
- (c) *Huonesha hali ya mzungumzaji kwa wakati huo kama hasira, huzuni, furaha na kothalika.*
- (d) *Hutolewa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo..... yea ni yule mzungumzaji huwasukisha yijumbe kipitia mdomo.*
- (e) *Inaweza kubadilika kutokana na mazingira kwa sababu hutolewa kwa njia ya mazungumzo ya mdomo.*

Kielelezo 6.3: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili*

Kielelezo 6.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyefafanua kwa usahihi sifa tano za lugha ya kimazungumzo (a) hadi (e) na kupata alama zote.


2.4 SEHEMU D: FASIHI KWA UJUMLA

Sehemu hii ilikuwa na maswali matatu ambayo yalimtaka mwanafunzi kutumia maarifa aliyojifunza katika kueleza dhima za fasihi, kukamilisha methali na kuonesha nafasi ya ngonjera kama maigizo na mashairi.

2.4.1 Swali la 7: Fasihi kwa Ujumla

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi kwa Ujumla* na mada ndogo ya *Dhima za Fasihi* na lililenga kupima tathmini. Swali lilimtaka mwanafunzi kueleza dhima kuu tano za fasihi na ilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 96.6 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji na ilikuwa mionganini mwa maswali yaliyojibiwa vizuri na wanafunzi wengi. Kiwango cha kufaulu katika swali hili kilikuwa ni kizuri ambapo asilimia 66.5 walipata alama za juu na za wastani. Chati Na. 6 inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.



Chati Na. 6: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 7

Chati Na. 6 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi ambapo, wanafunzi 276,272 (50.1%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6, wanafunzi 184,733 (33.5%) walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5 na wanafunzi 90,436 (16.4%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10.

Wanafunzi wengi (50.1%), waliofaulu kwa kiwango cha wastani walishindwa kueleza kwa usahihi dhima za fasihi kwa baadhi ya vipengele. Baadhi yao waliandika *dhima za misimu* na wengine waliandika *kazi za tamathali za semi* kama vile, *kupamba lugha* na *kuficha ukali wa maneno* kinyume na matakwa ya swali. Kielelezo 7.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyetao majibu yasiyojitosheleza katika swali hili.

7. Eleza kwa ufupi dhima kuu tano za fasihi.

- (i) Fasihi huburudisha, hii hutokana na kwamba Inauatira.....
hisha hadhira kwa namna kuma Nyimbo na maigizo:.....
- (ii) Fasihi hukemea marovu na hupatia watu maadili, hii ni kua.....
sababu Inavipengele rinavyodabuhajamii kama ushaini na Maigizo.....
- (iii) Fasihi huittambulisha jamii fulani ya watu hi, ni kua.....
sababu fasihi huwezesha kutufautuba jamii Mfano Ngomaya..... *Mgari*
- (iv) Fasihi hutunza historia ya jamii hii ni kua sababu.....
fasihi Inawezekuambatanishwa na historia kama Hadithi za Tarishi.....
- (v) Fasihi huwezesha watu kupata kipato chao, hii ni kua.....
sababu kazi hizi huyuktasana watu na hivyo huzwa, kupwetu riziki.....

Kielelezo 7.1: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama za wastani katika swali la 7*

Kielelezo 7.1 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeleza kwa usahihi dhima tatu za fasihi katika vipengele (i), (ii), (iv) na kueleza kimakosa faida mbili za fasihi katika vipengele (iii) na (v), hivyo kupata alama za wastani.

Hata hivyo, wanafunzi wachache, (16.4%) waliofaulu kwa kiwango kizuri cha alama 6.5 hadi 10 walikuwa na maarifa ya kutosha kuhusu dhima za fasihi katika jamii kama vile: *kuwasilisha mawazo/fikra za mtunzi/jamii, kuelimisha jamii, kusisimua/kuburudisha jamii, kuendeleza/kukuza lugha, kurithisha amali za jamii/utamaduni na kuadilisha jamii*. Kielelezo 7.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili.

7. Eleza kwa ufupi dhima kuu tano za fasihi.
- (i) *Fasihi hukurza lugha; Kuasababu fasihi huweza kuleta maneno mapya yanayo humika wakati wa utumiaji wa lugha.....*
 - (ii) *Fasihi huelimisha jamii; mfano Kwa nija ya mashairi na nyimbo jamii huelimika kutoKana na mazingira wanayoishi.....*
 - (iii) *Fasihi hufunza na Kuonya; mafunzo hayo hufikishwa Kuonye jamii ili Kuonya na matalizi tofauti wanayo kumbuka myo.....*
 - (iv) *Hiburudisha; fasihi huburudisha watu kutoKana na vifengele vyake kama hadithi hata pia mashairi.....*
 - (v) *Huendeleza maendeleo Katika jamii; fasihi hukamiasisha ukaji wa maendeleo kutoKana na ujumbe unapotikana.....*

Kielelezo 7.2: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyepeata alama za juu*

Kielelezo 7.2 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyeleza vizuri dhima tano za fasihi katika jamii na kupata alama za juu japokuwa hoja ya (v) ilikuwa na mapungufu na hivyo kutopata alama zote za swali.

Kwa upande mwingine, asilimia 33.5 ya wanafunzi waliokuwa na kiwango hafifu cha kufaulu walikuwa na uelewa mdogo kuhusu dhima za fasihi. Miongoni mwao, asilimia 15.1 walipata alama 0 kwa kuwa walishindwa kueleza dhima yoyote ya fasihi katika jamii kutokana na kukosa

uelewa wa vipengele anuwai nya kifasihi na hivyo kutoa majibu yasiyolingana na matakwa ya swali. Kwa mfano, baadhi yao walibainisha vipengele nya *fani* na *maudhui* katika fasihi na wengine walitaja baadhi ya tanzu na vipera nya fasihi simulizi kama vile *hadithi*, *methali*, *vitendawili*, *ngano*, kinyume na matakwa ya swali. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitaja vipengele nya *fani* katika kazi za fasihi na kutoa maelezo yasiyohusiana na vipengele hivyo kama kielelezo 7.3 kinavyodhahirisha.

7. Eleza kwa ufupi dhima kuu tano za fasihi.

- (i) Muundo - Husaidic kupangilic. Kahike mpangilio ulia..
mazuri. Kahike fasihi.....
- (ii) Mtindo - Husaidic. Kuweke. dzani mbalimbali za
Kazi za fasihi.....
- (iii) Wahusika - Husaidic. Kupangc matumatumizi..
yalivo. mazuri. katika. fasihi.....
- (iv) Matumizi ya lugha - Husaidic. baadhi ya jamii.
Kijifunze. lugha ya. Kigeni.....
- (v) Falsafa - Ni ile ambayo. kuandikwa. we
Usahihiki belc. Kukosec.....

Kielelezo 7.3: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyo sahihi*


Kielelezo 7.3 kinaonesha majibu ya mwanafunzi aliyelezea vipengele nya *fani* na *maudhui* kama vile: (i) *Muundo*, (ii) *Mtindo*, (iii) *Wahusika*, (iv) *Matumizi ya lugha* na (v) *Falsafa* kinyume na matakwa ya swali huku akitoa maelezo yasiyo na maana halisi ya kifasihi katika vipengele hivyo na kupata 0.

2.4.2 Swali la 8: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Methali*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuunda dhana za kifasihi na lilimtaka mwanafunzi

kukamilisha methali alizopewa ambapo lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 99.8 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji na lilikuwa miongoni mwa maswali yaliojibiwa vizuri zaidi na wanafunzi wengi. Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika swali hili kilikuwa ni kizuri ambapo asilimia 96.9 walipata alama za juu na za wastani. Chati Na. 7 inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.



Chati Na. 7: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 8

Chati Na. 7 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi ambapo, wanafunzi 368,037 (64.6%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6, wanafunzi 184,019 (32.3%) walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10 na wanafunzi wachache (17,661) sawa na asilimia 3.1 walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5.

Wanafunzi wengi (64.6%) waliojibu swali hili walifaulu kwa kiwango cha wastani kutokana na kukamilisha baadhi ya methali kwa usahihii na kushindwa kukamilisha methali nyingine walizopewa. Kwa jumla, wanafunzi hao walishindwa kuhusisha maumbo ya methali hizo na maana zake. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alikamilisha methali katika vipengele (a) Hakuna masika *yasiyo na ncha*; akihusisha na

methali *hakuna mrefu yasiyokuwa na ncha* badala ya ‘Hakuna masika *yasiyokuwa na mbu*’ na kutumia ukanushi katika kipengele (b) Mchonga mwiko *si mtumiaji* badala ya ‘Mchonga mwiko *hukimbiza mkonowe*’. Aidha, mwanafunzi huyo alikamilisha kwa usahihi methali katika vipengele (c) Chanda chema *huvikwa pete*, (d) Asiyefunzwa na mamaye *hufunzwa na ulimwengu* na (e) Dalili ya mvua *ni mawingu*; hivyo kupata alama za wastani. Kielelezo 8.2 kinadhihirisha majibu ya mwanafunzi huyo.

8. Kamilisha methali zifuatazo:

- (a) Hakuna masika..*yasiyokuwa na ncha*.....
- (b) Mchonga mwiko..*si mtumiaji*.....
- (c) Chanda chema.*huvikwa pete*.....
- (d) Asiyefunzwa na mamaye.*hufunzwa na ulimwengu*.....
- (e) Dalili ya mvua..*ni mawingu*.....

Kielelezo 8.2: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi yasiyojitosheleza*

Kwa upande mwingine, asilimia 32.3 ya wanafunzi waliofaulu kwa kiwango kizuri swali hili walikuwa na uwezo wa kutambua miundo ya methali na hivyo kuweza kukamilisha methali walizopewa kwa usahihi. Kwa jumla, methali zote zilikuwa zinafungamana na mazingira na hivyo kuwa rahisi katika kubaini upande wa pili wa methali husika. Kielelezo 8.1 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili.

8. Kamilisha methali zifuatazo:

- (a) Hakuna masika.....*Yas!yo na mbu.*.....
- (b) Mchonga mwiko.....*hukimbiza mkenaue.*.....
- (c) Chanda chema.....*huvishwa pete.*.....
- (d) Asiyefunzwa na mamaye.....*hufuzwa na Ulimwengu.*.....
- (e) Dalili ya mvua.....*Ni Mawingu!*.....

Kielelezo 8.1: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu kwa usahihii swali la 8*

Licha ya kiwango kizuri cha kufaulu, wanafunzi wachache (3.1%) walishindwa kujibu swali hili na hivyo kupata alama hafifu. Wanafunzi hao walionesha hali ya kutokuwa na maarifa ya kutosha kuhusu miundo ya methali na hivyo kushindwa kukamilisha methali walizopewa. Kwa jumla, wanafunzi hao walishindwa kutambua mazingira halisi ya methali hizo na hivyo kuwa vigumu kubaini upande wa pili wa methali husika. Baadhi yao waliandika kauli zinazopingana na kauli ya awali ya methali husika kama vile: (a) Hakuna masika *hakuna mvua*, (b) Mchonga mwiko *ndo mla chakula*, (c) Chanda chema *chakuita peponi*, (d) Asiyefunzwa na mamaye *hufunzwa na babaye* na (e) Dalili ya mvua *jua*. Aidha, wanafunzi wengine waliandika kauli zisizo na uhusiano wowote na methali husika kama kielelezo 8.3 kinavyoonesha majibu ya mwanafunzi aliyeshindwa kukamilisha methali hata moja na kupata alama 0.

8. Kamilisha methali zifuatazo:

- (a) Hakuna masika.....*giza nzito*.....
- (b) Mchonga mwiko.....*haina asara*.....
- (c) Chanda chema.....*awe mwemaa*.....
- (d) Asiyefunzwa na mamaye.....*ndo babaye*.....
- (e) Dalili ya mvua.....*chumui njingi*.....


Kielelezo 8.3: *Sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejepata alama hafifu*

Kielelezo 8.3 kinaonesha sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejamiliwa methali kwa kuandika maneno yasiyohusiana na kauli za methali (a) hadi (e) na kupata 0.

2.4.3 Swali la 9: Fasihi Simulizi

Swali lilitoka katika mada ya *Uhakiki wa Kazi za Fasihi Simulizi* na mada ndogo ya *Uhakiki wa Ushairi na Maigizo*. Swali lililenga kupima uwezo wa mwanafunzi wa kuchambua na lilikuwa na vipengele viwili na lilimtaka mwanafunzi kutoa sababu tatu kwa kila kipengele (i) kuthibitisha usemi kuwa "ngonjera ni maigizo" na (ii) kuthibitisha usemi kuwa "ngonjera ni mashairi." Swali hili lilikuwa na jumla ya alama 10.

Swali hili lilijibiwa na asilimia 93.6 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji, idadi inayoonekana kuwa pungufu kidogo ikilinganishwa na maswali mengine kutokana na umahiri mdogo wa wanafunzi katika miundo ya ushairi na maigizo. Swali hili lilikuwa na kiwango cha chini zaidi cha kufaulu ambapo asilimia 25.3 pekee ndio walioweza kujibu swali hili kwa kiwango kizuri na cha wastani. Chati Na. 8 inaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi katika swali hili kwa asilimia.



Chati Na. 8: Asilimia ya Kufaulu kwa Wanafunzi katika Swali la 9

Chati Na. 8 inaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi ambapo, wanafunzi wengi, (399,322) sawa na asilimia 74.7

walikuwa na kiwango hafifu cha alama 0 hadi 2.5. Aidha, wanafunzi 120,812 (22.6%) walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 3 hadi 6 na wanafunzi wachache (14,433) sawa na asilimia 2.7 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 6.5 hadi 10.

Wanafunzi wengi (74.7%) waliojibu vibaya swali hili walipata alama za chini kuanzia 0 hadi 2.5, mionganoni mwao, asilimia 47.5 walipata 0 kutokana na kushindwa kueleza sababu hata moja zinazofanya ngonjera kuwa kama *maigizo* na pia kama *mashairi* kwa kuwa walikosa maarifa kuhusu *ngonjera*, *maigizo na mashairi*. Baadhi yao, walielezea dhima za fasihi kama vile: *huelimisha jamii*, *huburudisha jamii*, *huonya jamii*, *huadabisha jamii* na nyinginezo. Wanafunzi wengine walitoa sababu za kutofautisha vipengele hivyo ambapo ngonjera kuwa kama ‘*mashairi*’ walielezea *uwepo wa majibzano ya wahusika* ambapo kiuhalisia *mashairi* hayana wahusika bayana wanaoweza kujibizana. Pia ngonjera kuwa kama ‘*maigizo*’ walielezea *uwepo wa idadi ya mistari/ubeti* ambapo kiuhalisia *maigizo* huundwa na masimulizi ya kupokezana kati ya mhusika mmoja na mwingine tofauti na mistari/ubeti. Wanafunzi hao walitakiwa kutoa sababu za ngonjera kuwa *maigizo* kama vile; *ina utendaji ndani yake, huwa na wahusika zaidi ya mmoja na ina muktagha au jukwaa la uigizi*; ngonjera kuwa *mashairi* kama vile: *inafuata urari wa vina na mizani, huwa katika muundo wa beti tofauti tofauti na ina vipande mstari viwili*. Kielelezoo 9.1 ni mfano wa jibu la mwanafunzi aliyeshindwa kujibu swali hili.

9. (i) Ngonjera ni maigizo kwa sababu:

- Hu ulimila jamii. Ikiupilia maigizo, na mashairi
hakikiko Umbaya wa nafungo jihili / Ngonjera
kubuji mada fulani / piazi mtaa yote hili
pupa hukwaa yule.
- Hukurudu ha jamii kua. Hukuzo maigizo
mashairi mianzi amezaa mi wani
Inamaana amelewa kufinduliwa.
- Hukoo yuizi juu ya jamii kua upumla.
Inaweza kufaa yuizi ambayo jamii inaweza kufaa
zaidi; kufamfano mchumia jidni hili hivutini.

(ii) Ngonjera ni mashairi kwa sababu:

- Nyanya na kufadabuha jamii, ngonjera
Inatumtha kuonya jamii kua. Maigizo lau
maigizo uwanayotaka tiba, mpano michelka
mujalma kuhla hukla mwenyewe.
- Kufanya amali za jamii nzima, kufisha
mawimilizi wanayotaka wanarengela barmye...
na. Wanafunzi hao na ufunga, mkuu. Hukubu haozi
Hukoo na hili.
- Hukoo hili ha jamii kua inzi inayobilita kua
Uwanayotaka wa ngonjera pemanya na ukurasi wahe-
miano. Iwanayotaka mto wapo, wanafunzi
Hukoo na hili.

Kielelezo 9.1: *Sampuli ya jibu la mwanafunzi aliyejibu vibaya swali la 9*

Kielelezo 9.1 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika dhima mbalimbali za fasihi katika jamii badala ya kutoa sababu za ngonjera kuwa kama *maigizo* au *mashari* kinyume na matakwa ya swali.

Licha ya swali hili kujibiwa vibaya na wanafunzi wengi, asilimia 22.6 waliweza kujibu swali hili na kufaulu kwa kiwango cha wastani. Wanafunzi hao waliweza kutoa sababu za ngonjera kuwa kama *maigizo* au *mashari* kwa baadhi ya vipengele na kutoa majibu yasiyojitosheleza katika vipengele vingine. Aidha, wapo wanafunzi wachache (2.7%) waliofaulu kwa kiwango kizuri kwa kuwa walikuwa na umahiri na uelewa wa kutosha kuhusu *ngonjera*, *maigizo na mashairi*, hivyo kupata alama za juu kuanzia 6.5 hadi 10. Wanafunzi hao walikuwa na uwezo wa kutambua miundo na uwasilishaji wa ngonjera, mashairi na maigizo. Wanafunzi hao waliweza

kuthibitisha kwa kutoa sababu sahihi katika (i) ngonjera ni maigizo kwa kuwa: *Ina utendaji ndani yake, huwa na wahusika zaidi ya mmoja na ina muktadha au jukwaa la uigizi* na (ii) ngonjera ni mashairi kwa kuwa: *Inafuata urari wa vina na mizani, huwa katika muundo wa beti tofauti tofauti na ina vipande mstari viwili*. Kielelezo 9.2 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyejibu vizuri swali hili.

9. "Ngonjera ni maigizo na pia ni mashairi". Toa sababu tatu za kuthibitisha usemi huo.

(i) Ngonjera ni maigizo kwa sababu:

- *Ina.....utendaji.....ndani.....yake:.....yaani.....watu.....wanotambaa.....wanaweka.....kujigiza.....au.....kutenda.....vitendo.....vya.....ngonjera.....hiya.....*
- *Huwa.....na.....wahusika.....zaidi.....ya.....mmoja.....dm.....bao.....hiitambaa.....kama.....igiza.....*
- *Ina.....muktadha.....au.....jukwaa.....la.....uigizi.....*

(ii) Ngonjera ni mashairi kwa sababu:

- *Inafuata.....urari.....wa.....vina.....na.....mizani.....Mfano:.....Hadi.....hadi.....naingia.....mhale.....peru.....ninasongo.....wtate.....nawasilimise.....ninamengi.....ya.....kugango.....*
- *Huwa.....katika.....muundo.....wa.....beti.....tofauti.....tofauti:.....*
- *Ina.....vipande.....mstari:.....viwili.....kama.....muundo.....wa.....shairi.....ulixya.....ambapo.....kila.....kiparade.....mstari.....moxaa.....mifungo:.....huwa.....na.....mizani.....name.....*

Kielelezo 9.2: *Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 9*

Kielelezo 9.2 kinaonesha sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi aliyetoa sababu tatu sahihi kwa kila moja ili kuthibitisha kuwa (i) Ngonjera ni maigizo na (ii) Ngonjera ni mashairi.

2.5 SEHEMU E: UANDISHI WA INSHA/UTUNGAJI

Sehemu hii ilikuwa na swali moja na lilimtaka mwanafunzi kuandika insha isiyopungua maneno mia moja na hamsini (150) na isiyozidi maneno mia mbili (200).

2.5.1 Swali la 10: Uandishi wa Insha

Swali lilitoka katika mada ya *Uandishi* na mada ndogo ya *Uandishi wa Insha* na lililenga kupima uundaji. Swali lilimtaka mwanafunzi kuzingatia hoja nne katika kuandika insha isiyopungua maneno mia moja na hamsini (150) na isiyozidi maneno mia mbili (200) kuhusu "Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili" na ilikuwa na jumla ya alama 15.

Swali hili lilijibowi na wanafunzi 548,309 sawa na asilimia 96.0 ya wanafunzi wote waliofanya upimaji huu. Swali hili ilikuwa mionganoni mwa maswali yaliyokuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo asilimia 54.7 walifaulu kwa kiwango kizuri na cha wastani. Jedwali Na. 2 linaonesha viwango vya kufaulu vya wanafunzi kwa asilimia.

Jedwali Na. 2: Kufaulu kwa Wanafunzi kwa Asilimia

Alama	Idadi ya Wanafunzi	Asilimia ya Wanafunzi
0.0 - 4.0	248,384	45.3
4.5 - 9.5	214,937	39.2
10 - 15	84,988	15.5

Jedwali Na. 2 linaonesha kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi ambapo, wanafunzi 248,384 (45.3%) walikuwa na kiwango hafifu cha kufaulu cha alama 0 hadi 4. Aidha, wanafunzi 214,937 sawa na asilimia 39.2 walifaulu kwa kiwango cha wastani kwa kupata alama kuanzia 4.5 hadi 9.5 na wanafunzi wachache (84,988) sawa na asilimia 15.5 walifaulu kwa kiwango kizuri kwa kupata alama kuanzia 10 hadi 15.

Wanafunzi 214,937 (39.2%) waliofaulu kwa kiwango cha wastani waliandika insha isiyojitosheleza. Baadhi yao

waliandika insha isiyozingatia utangulizi na katika kiini wengine walitoa hoja zisizojitosheleza kiufafanuzi. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja alitoa hoja kama vile *Lugha ya Kiswahili ni nyenzo ya mawasiliano, kitambulisho cha nchi, hudumisha utamaduni* na kuongeza hoja ya *hurahisisha kupashana au kupeana habari* ambayo ni marudio ya hoja ya kwanza *nyenzo ya mawasiliano* hivyo kupata alama za wastani.

Aidha, wanafunzi wachache 84,988 sawa na asilimia 15.5 waliojibu swali hili walifaalu kwa kiwango kizuri na kupata alama za juu kutokana na kuwa na uelewa wa kutosha kuhusu uandishi wa insha. Wanafunzi hao waliandika insha kwa kuzingatia kichwa cha insha, mwanzo wa insha, kiini cha insha na mwisho wa insha. Aidha, katika kiini waliweza kuelezea umuhimu wa lugha ya Kiswahili kwa jamii kama vile kutumika katika: *kuwasiliana, kutolea mafunzo, kutambulisha jamii, kuhifadhi, kueneza utamaduni na kukuza umoja na ushirikiano baina ya watumiaji*. Kielelezo 10.1 ni sampuli ya majibu ya mwanafunzi aliyeandika insha kwa usahihi.

10. Kwa kuzingatia hoja nne, andika insha isiyopungua maneno mia moja na hamsini (150) na isiyozidi maneno mia mbili (200) kuhusu Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili.

UMUHIMU WA LUGHA YA KISWAHILI

Lugha ni mfumo uo cauti za nabolu zenyé kubeba mnana zilitzakubaliwa na jomii za watu fulani ili zitumike katika mawasiliano. Lugha ya Kiswahili ni lugha maalum inayotumika na watanzania wote lugha ya Kiswahili ina nyanya mbili nazo ni lugha ya mozungumzo na lugha ya maandishi. Pia lugha ya Kiswahili ina tanzu mbili nazo ni Somu no Fasili.

Hoja zifualazo zinaonyesha umuhimu uo lugha ya Kiswahili.

Lugha ya Kiswahili hutumika katika mawasiliano watu mbali mbali hasi watanzania hutumia lugha ya Kiswahili ili Kupashana haleni, Kizungumzo, Kyujuliona hali na kuvawiliano. Njia za mawasiliano zinrotumia lugha ya Kiswahili ni pamoja na magoraji, Bonua za Kirafiki, Bonua zo Kikazi na Rusinga. Lugha ya Kiswahili ni muhimu sand koo mawasiliano kuani lugha hiyo hutumiwa na watanzania wengi.

Lugha ya Kiswahili hutumika katika kutolea mafunzo, vituo mbali mbali vya kutolea mafunzo ikiwemo shule za senkeli, hutumia lugha ya Kiswahili katika kutolea mafunzo. Mafunzo hayo husaidia katika upatikanaji uo ajira na hiryo, uchumi uo nchi huongezeka koo horaka.

Lugha ya Kiswahili hutumika kama kitambulisho cho watanzania, kuani watanzania wengi hutambulika koo kuongea lugha yao ya taifa ambayo ni Kiswahili. Kutokana na utandauzaji na ukujaji uo sayansi na teknolojia, watu wamekuwa wakizungumza na kujifuriza lugha mbali mbali. Ito lori mo kuu na lugha ambayo humtambulisha mtu taifa alilotoka. Lugha ya Kiswahili huwatambulisha watanzania wote.

lugha yo Kiswahili hutumiko
 Kuharaka uchirikiano baina ya waana jamii, Kwani ushirkiano
 huchangia katika ukujji wa uchumi wa nchi, lugha yo kiswahili
 huhamisisha ushirkiano Kwani wasanii mbalimbali hutunia
 Kiswahili ili Kutunga nyimbo no nganjera mbali mbali. Kuhusu
 umuhimu wa ushirkiano baina ya watanzania au wanganui
 Kijumla lugha yo kiswahili ina dhima nyingo-
 nezo, kiwemo kritunzo amali zo jamii. Ili watumigaji coo lugha
 ya kiswahili cweweze kuitumia lugha hiyo kua upasaho zaidi,
 wanatakiwa wapewate tonatibu zote zo lugha hiyo kimaona,
 Kimuundo, kimatamshi no kimantiki.

Kielelezo 10.1: Sampuli ya jibu zuri la mwanafunzi katika swali la 10

Kielelezo 10.1 kinaonesha sampuli ya jibu la mwanafunzi aliweza kuandika insha yenye utangulizi mzuri, kutoa hoja nne katika kiini zinazoelezea ‘Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili’ na kutoa hitimisho zuri linaloendana na kiini cha insha; hivyo kupata alama za juu.

Kwa upande mwengine, wanafunzi 248,384 sawa na asilimia 45.3 waliofaulu kwa kiwango hafifu walikosa maarifa na uelewa kuhusu uandishi wa insha. Baadhi yao waliandika barua mfano, mwanafunzi mmoja aliandika barua yenye kichwa cha barua 'UMUHIMU WA LUGHA YA KISWAHILI' na wengine walitunga habari/insha mbalimbali zisizohusiana na kichwa cha insha walichopewa. Kwa mfano, mwanafunzi mmoja aliandika insha iliyozungumzia mambo mbalimbali anayotakiwa kufanya mwanafunzi akiwa shulen kama vile; *awe na daftari na sare za shule, ajue anachofundishwa, aweze kufafanua jambo, ajue umuhimu wa shule, azingatie muda, awe na nidhamu, apate adhabu, afanye kazi kwa bidii na aulize maswali darasani*, badala ya kuandika insha inayohusu 'Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili' kama swali lilivyotaka.

10. Kwa kuzingatia hoja nne, andika insha isiyopungua maneno mia moja na hamsini (150) na isiyozidi maneno mia mbili (200) kuhusu Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili.

MWANAFUNZI NA DAFTARI,

Mwanafunzi anafakira auie na dafuta
kifaa kila somo ilii auzeze kufikia kumbusho
alicycfundishaa na uhalifu.

Mwanafunzi ne muhimu kuyuuwa nana choco
fundehuici na uhalimu kifamusadra kaffka maliha
yake au mithoni yake.

Mwanafunzi anafakira kufafanua njambo
alikofundeshua na muhalimu hirojambu alauasa
Idhaumenzake kuiiafanulia kuna undani za idha.

Mwanafunzi anafakira auue umuhimu
uake auie kufikia shule na na kufubla alichole
tua shulenii.

Mwanafunzi anafakira auie na sale
za shule ilii auzeze kuvali kaffka mazingira hayo.

Mwanafunzi anafakira aringote muda
wa kufikia shulenii afanyi usafiri angre Darasani
Kuajiri ya vifundi mdalimi mwanafunzi hataku
uue kautoka tukia nje uakata uci vifundi.

Mwanafunzi anafakira auie na nitharau
auie muonye kudhura jambo auie muoneye
busara ati amyle za shule auie muonye.

Kielelezo 10.3: *Sehemu ya jibu la mwanafunzi aliyepata alama hafifu*

Kielelezo 10.2 kinaonesha jibu la mwanafunzi aliyeandika insha isiyozingatia kichwa cha insha alichopewa yaani "Umuhimu wa Lugha ya Kiswahili" badala yake akaandika "MWANAFUNZI NA DAFTARI" kinyume na matakwa ya swalii.

3.0 UCHAMBUZI WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MADA

Uchambuzi uliofanyika katika somo la Kiswahili unaonesha kuwa, wanafunzi wengi walifaulu kwa kiwango cha wastani katika mada nyingi zilizopimwa kwa mwaka 2019. Hata hivyo, takwimu zinaonesha kuwa, katika upimaji huu mada ya *Ufahamu* pekee ndiyo iliyokuwa na kiwango kizuri cha kufaulu (84.5%) ikiwa pungufu kidogo kwa asilimia 0.5 ikilinganishwa na kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2018 (85%). Uchambuzi huu unaonesha kuwa, katika somo la Kiswahili wanafunzi wana umahiri wa juu kuhusu mada hii kwa kuwa imekuwa na kiwango kizuri cha kufaulu kwa mfululizo wa miaka mitatu ambapo kwa mwaka 2017, kiwango cha kufaulu katika mada hiyo kilikuwa (72.45%).

Aidha, mada nyingine zote zilikuwa na kiwango cha wastani cha kufaulu ambapo mada ya *Sarufi* (63.1%) ikiwa na ongezeko la asilimia 14.7, ikifuatiwa na Fasihi kwa Ujumla (62.9%) ikiwa na upungufu wa asilimia 9, ikifuatiwa na mada ya *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (62.2%) ikiwa na ongezeko la asilimia 7.8 na *Uandishi* ikiwa na ongezeko kubwa la asilimia 21.8 zikilinganishwa na viwango vya kufaulu vya mada hizo kwa mwaka 2018.

Wastani wa kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika mada zote kwa mwaka 2019 ni asilimia 65.48, kiwango ambacho ni cha juu kwa asilimia 6.96 ikilinganishwa na mwaka 2018 ambapo wastani wa kiwango cha kufaulu kwa mada kilikuwa 58.52%. Kiwango cha kufaulu kwa mwaka 2019 kinadhihirisha kuwa, wanafunzi wengi walikuwa na maarifa ya wastani katika mada mbalimbali zilizopimwa na hivyo kutoa majibu yasiyoyitotesheleza kwa maswali mengi na kufaulu kwa kiwango cha wastani. Hata hivyo, ongezeko la asilimia 6.96 la kiwango cha kufaulu katika mada zilizopimwa linaonesha kuwa zipo jitihada za makusudi zilizofanywa katika mchakato mzima wa ujifunzaji na ufundishaji wa mada hizo.

Licha ya kiwango cha wastani cha kufaulu katika mada nyingi kwa mwaka 2019, mada ya *Uandishi wa Insha* ilikuwa na kiwango cha chini kuliko nyingine kutokana na wanafunzi wengi kukosa maarifa na ujuzi wa kutosha kuhusu uandishi wa insha. Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi katika mada mbalimbali kwa mwaka 2019 kimeainishwa katika **Kiambatisho A**. Pia

ulinganifu wa viwango vya kufaulu vya wanafunzi katika mada kwa mwaka 2018 na 2019 umeainishwa katika **Kiambatisho B.**

4.0 HITIMISHO

Upimaji wa Kidato cha Pili kwa mwaka 2019 katika somo la Kiswahili ulizingatia muhtasari wa somo la Kiswahili na maswali yote yalipimwa kwa kuzingatia majazi ya utambuzi ambayo ni *maarifa, ufahrenu, utumizi, uchambuzi, uundaji na tathmini*. Kiwango cha kufaulu cha wanafunzi kilikuwa kizuri ambapo asilimia **92.19** walipata alama 30 na zaidi.

Uchambuzi huu unaonesha changamoto mbalimbali kama vile, wanafunzi wengi kutokuwa na uelewa wa kutosha kuhusu mada mbalimbali zilizofanyiwa upimaji kama vile *Sarufi, Fasihi kwa Ujumla, Uandishi, Mawasiliano na Utumizi wa Lugha*. Pia, baadhi ya wanafunzi kutofuata maelekezo ya maswali ipasavyo. Changamoto hizo hazina budi kutatuliwa ili kuinua kiwango cha kufaulu kwa wanafunzi katika somo la Kiswahili kama vile; wanafunzi kupewa mazoezi ya kutosha na ya mara kwa mara kuhusu uandishi wa insha. Pia, kuwe na msisitizo wa matumizi ya lugha fasaha ili kuondokana na madhara ya kutumia lugha isiyo fasaha katika kujibu maswali mbalimbali. Aidha, wanafunzi sharti wapatiwe mazoezi ya kutosha ya kisarufi ili kuwajengea weledi katika mada ya *Sarufi* hususan aina za maneno. Pia, wanafunzi wapewe mazoezi zaidi ya utunzi wa kazi mbalimbali za fasihi simulizi kama vile methali, ngonjera, mashairi na maigizo ili kuwajengea ujuzi wa kutumia kanuni anuwai za utunzi wa kazi za kisanaa.

Hata hivyo, uchambuzi huu unaonesha kuwa zipo jitihada kubwa zilizofanyika katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hii ni kwa sababu viwango vya kufaulu kwa mwaka 2019 vya mada za *Sarufi* (63.1%), *Mawasiliano na Utumizi wa Lugha* (62.2%) na *Uandishi* (54.7%) vimekuwa vya juu ikilinganishwa na mwaka 2018 ambavyo vilikuwa (48.4%), (54.4%) na (32.9%) mtawalia. Aidha, mada ya *Fasihi kwa Ujumla* (62.9%) imekuwa na kiwango cha chini kidogo cha kufaulu kwa mwaka 2019 ikilinganishwa na mwaka 2018 ambapo kiwango cha kufaulu kilikuwa (71.9%). Kushuka kwa kiwango cha kufaulu katika mada hii kumechangiwa na wanafunzi wengi (74.7%) kujibu vibaya swalı mojawapo katika mada hii (swali la 9) na kuwa na kiwango hafifu cha kufaulu.

Mwisho, taarifa hii ya uchambuzi wa majibu ya wanafunzi kuhusu upimaji wa Kidato cha Pili inatarajiwa kuwa chachu na dira ya mabadiliko kutoka kiwango cha wastani cha kufaulu na kuwa kiwango kizuri cha kufaulu katika mada mbalimbali za somo la Kiswahili. Hata hivyo, hii itasaidia kutatua changamoto kwa walimu na wanafunzi katika suala zima la ufundishaji na ujifunzaji wa mada mbalimbali. Hivyo, uchambuzi huu utawawezesha kuelewa makosa mbalimbali yanayosababisha kiwango hafifu cha kufaulu kwa baadhi ya mada ili kuinua zaidi kiwango cha kufaulu katika upimaji na mitihani mbalimbali ya somo la Kiswahili.

5.0 MAONI NA MAPENDEKEZO

Ili kuinua kiwango cha kufaulu katika somo la Kiswahili inapendekezwa kuwa:

- (a) Walimu wasisitize wanafunzi kutilia mkazo katika kujifunza mada za *Mawasiliano na Utumizi wa Lughha, Fasihi kwa Ujumla, Sarufi* pamoja na *Uandishi wa Insha* kwani ni mada ambazo baadhi ya wanafunzi wameonesha uwezo mdogo wa kuelewa katika kujibu maswali husika.
- (b) Serikali na wadau wengine wanaoshughulikia elimu waweke na kusimamia mifumo ya uingizaji na matumizi ya vitabu vyta kiada vinavyotumika katika kufundishia na kujifunzia somo la Kiswahili katika shule za Sekondari nchini Tanzania ili kusawazisha mada kulingana na mtaala wa ufundishaji/ujifunzaji kwa somo la Kiswahili.
- (c) Matumizi ya lugha fasaha ya Kiswahili yasisitizwe kwa wanafunzi katika mazungumzo na maandishi yao ya kila siku ili kuifanya lugha ya Kiswahili kukua na kuenea zaidi.
- (d) Walimu watumie njia ya majadiliana na onesho mbinu katika kufundisha mada ya Uandishi wa Insha ili kuwajengea wanafunzi uwezo wa kujieleza kimantiki na kwa ufasaha.
- (e) Walimu watumie mbinu shirikishi na mazoezi ya mara kwa mara katika ufundishaji na ujifunzaji wa mada za *Sarufi, Fasihi kwa Ujumla, Mawasiliano na Utumizi wa Lughha* ili kuwajengea wanafunzi msingi mzuri wa maarifa katika mada hizo.

KIAMBATISHO A

**UCHAMBUZI WA KIWANGO CHA KUFAULU KWA WANAFUNZI
KATIKA MADA KWA MWAKA 2019**

Na.	Mada	Kufaulu kwa kila Swali		Wastani wa Kufaulu (%)	Maoni
		Na. ya Swali	% ya Kufaulu (alama 30+)		
1	<i>Ufahamu</i>	1	91.5	84.5	Vizuri
		2	77.5		
2	<i>Sarufi</i>	3	66.1	63.1	Wastani
		4	60.1		
3.	<i>Fasihi kwa Ujumla</i>	7	66.5	62.9	Wastani
		8	96.9		
		9	25.3		
4.	<i>Mawasiliano na Matumizi ya lugha</i>	5	94.3	62.2	Wastani
		6	30.1		
5.	<i>Uandishi wa Insha/Utungaji.</i>	10	54.7	54.7	Wastani

KIAMBATISHO B

ULINGANIFU WA VIWANGO VYA KUFAULU KWA WANAFUNZI KATIKA MADA KWA MWAKA 2018/2019

